**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**Alhamis, 02 Julai, 2026**
**Tanga Beach Resort.**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUWA MWENYEJI WA MKUTANO WA 12 WA NCHI WANACHAMA WA MKATABA WA NAIROBI (COP12), UNAOTEGEMEWA KUFANYIKA TAREHE 06-09 OKTOBA 2026, DAR ES SALAAM

---

***Mheshimiwa Balozi Batilda Buriani Mkuu wa Mkoa wa Tanga,***

***Ndugu Rashid Mchatta Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga,***

***Balozi Baraka Luvanda Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais,***

***Mhandisi Emigidius Kasuzu Katibu Tawala Msaidizi - Uchumi na Uzalishaji,***

***Viongozi wa Chama cha Mapinduzi,***

***Mwakilishi kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Zanzibar,***

***Mwakilishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),***

***Mwakilishi kutoka Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC)***

***Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais***

***Mwakilishi kutoka Wetland International***

***Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam***

***Watendaji na Maafisa mbalimbali wa Serikali,***

***Wawakilishi wa vikundi mbalimbali vya Uhifadhi wa Mazingira,***

***Ndugu wanahabari,***

***Wageni waalikwa,***

***Ndugu wananchi,***

***Mabibi na Mabwana,***

***Kazi na Utu!***

**Ndugu Wananchi,**

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo, kushuhudia tukio hili muhimu. Pia nawashukuru wote kwa kutenga muda wenu kuja kuungana nasi katika siku hii ya leo. Hakika ukubwa wa hadhira hii ni ishara tosha kuhusu utayari wa kuendeleza jukumu la kuhifadhi rasilimali ya Bahari ya hindi kwa maendeleo endelevu nchini.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa namna ya kipekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na maono yake makubwa katika kuipa kipaumbele Sekta ya Mazingira na uhifadhi wa rasilimali za bahari. Dhamira hiyo imejidhihirisha kupitia hatua mbalimbali za Serikali za kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa rasilimali maji za Bahari, Mito, Maziwa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu.

Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imeitambua Sekta ya Uchumi wa Buluu, ambayo Mkataba huu umejikita, kuwa miongoni mwa sekta za kimkakati za kuleta mageuzi ya maendeleo endelevu yanayochangia ukuaji wa kijamii, kiuchumi na kiikolojia. Uchumi wa Buluu unahusisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kwa ajili ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Kwa kuwa Tanzania ni nchi ya pwani, ina fursa kubwa ya kunufaika na sekta hii kupitia maeneo mbalimbali ikiwemo uvuvi, nishati, usafirishaji, utalii, madini, mazingira na viwanda. Hivyo, Maamuzi na mwelekeo wa Serikali vinaendelea

kuiweka nchi yetu katika nafasi bora ya kufikia maendeleo endelevu yanayozingatia uhifadhi na matumizi sahihi ya rasilimali za bahari.

**Ndugu Wananchi,**

Napenda kutoa pongezi na shukrani nyingi kwenu nyote kwa kuitikia mwaliko wangu na kushiriki kikao hiki. Hakika, uwepo wenu ni ishara tosha ya utayari wenu wa kuendeleza jukumu letu la pamoja la kuhifadhi mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu. Ushirikiano wenu ni msingi muhimu katika kufanikisha azma hii ya kitaifa.

**Ndugu Wananchi,**

Napenda kuutaarifu Umma wa Watanzania kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) imechaguliwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP12), utakaofanyika tarehe 06-09 Oktoba 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Jijini Dar es Salaam (JNICC).

**Ndugu Wananchi,**

JMT ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Nairobi unaohusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi. Mkataba huu ulisainiwa tarehe 21 Juni 1985 na unatekelezwa chini ya usimamizi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP). Nchi wanachama hukutana kila baada ya miaka miwili kupitia Mkutano wa Nchi Wanachama (*Conference of Parties – COP*) kujadili utekelezaji wa shughuli, Mipango na Mikakati ya Mkataba.

Katika Mkutano wa 11 wa Nchi Wanachama (COP11) uliofanyika nchini Madagasca mwaka 2024, JMT ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Mkataba wa Nairobi (Chair of the Bureau) kwa kipindi cha miaka miwili hadi Disemba Mwaka 2026, pamoja na kuteuliwa kuwa mwenyeji wa COP12.

**Ndugu Wananchi,**

Mkutano wa COP12 utajadili utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mkataba kwa kipindi cha mwaka 2024–2026, kupokea taarifa za mapato na matumizi, pamoja na kujadili masuala muhimu ikiwemo:

- Hifadhi na urejeshwaji wa mifumo ikolojia ya bahari kama mikoko, miamba ya matumbawe na nyasi bahari;

- Kukabiliana na uchafuzi wa bahari, hususan taka za plastiki na kumwagika kwa mafuta;
- Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Bioanuai ya Bahari zilizo nje ya mamlaka ya kitaifa (BBNJ); na
- Kuimarisha Uchumi wa Buluu endelevu na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

**Ndugu Wananchi,**

Kaulimbiu ya kitaifa ya mkutano huu ni:
***"Towards a Sustainable Blue Economy in the Western Indian Ocean for People and Nature: A 40 - Year Journey"*** ambapo kwa lugha ya Kiswahili kauli mbiu hii inamaanisha ***"Kuelekea Uchumi wa Buluu Endelevu katika Ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi kwa Manufaa ya Watu na Mazingira ya asili: Safari ya Miaka 40."***

Pamoja na mambo mengine, Uenyeji wa mkutano huu una manufaa makubwa kwa Taifa letu, yakiwemo:

i. Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kinara wa diplomasia ya hifadhi ya rasilimali za bahari katika Ukanda wa Bahari ya Hindi;
ii. Kuvutia uwekezaji wa rasilimali za kifedha kwa miradi ya hifadhi ya rasilimali za bahari na uchumi wa buluu;
iii. Kujenga uwezo wa kitaifa katika kukabiliana na uchafuzi wa bahari na athari za mabadiliko ya tabianchi;
iv. Kukuza utalii wa mikutano na kuitangaza Tanzania kimataifa;
v. Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari.

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, na Washirika wa Maendeleo imeanza maandalizi rasmi ya mkutano huo, ikiwemo kuunda Kamati za Kitaifa na Kamati za Uratibu kwa ajili ya kuhakikisha mkutano unafanyika kwa mafanikio makubwa.

**Ndugu Wananchi,**

Natoa wito kwa wadau wote Wizara, Taasisi za Umma, Sekta Binafsi, Wanazuoni, Watafiti, Mashirika ya Kiraia na Wananchi kwa ujumla – kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mkutano huu. Ushiriki wenu utaimarisha mafanikio ya mkutano na kuongeza tija kwa Taifa letu.

Kwa pamoja, tuendelee kulinda na kuhifadhi rasilimali zetu za bahari na pwani kwa ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

**Imetolewa na:**
**Mhe. Reuben Nhamanilo Kwagilwa**
**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**